OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA SUMBAWANGA

SHULE YA SEKONDARI LUKANGAO,
S.L.P 471,
SUMBAWANGA.
TAREHE……

Kumb. Na LSS/12/2021/VOL.07
JINA LA MWANAFUNZI…….
S.L.P ……..
SUMBAWANGA.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LUKANGAO KWA MWAKA WA MASOMO 2021

1. Utangulizi

Ninayo furaha kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha Kwanza katika shule hii mwaka 2020. Shule ya Sekondari Lukangao ipo umbali wa kilometa 12 Kaskazini Magharibi toka Makao Makuu ya Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **11/01/2021**. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **1 /01/2021** (ndani ya siku saba).

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 Sare za Shule

(a) Wavulana

i. Suruali moja rangi ya **Bluu Bahari** na nyingine rangi ya **Damu ya Mzee**
ii. Mashati mawili meupe tetroni mikono mifupi
iii. Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga kwa kamba
iv. Sweta la Damu ya Mzee lenye ukosi wa V.
v. Tai moja ya Bluu bahari na nyingine ya Damu ya Mzee
vi. Soksi nyeusi jozi mbili

(b) Wasichana

i. Sketi moja ya Bluu Bahari na nyingine ya Damu ya Mzee
ii. Mashati mawili meupe tetroni mikono mifupi
iii. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba vyenye kisigino kifupi
iv. Tai moja ya Bluu Bahari na nyingine ya Damu ya Mzee
v. Soksi nyeupe jozi mbili
vi. Sweta la Damu ya Mzee lenye ukosi wa V.

(c) Kwa Waislam

Rangi ya hijabu ifanane na rangi ya sare ya shule.

(d) Sare ya michezo kwa shule hii ni:-

Wavulana:

i. Raba jozi moja
ii. Bukta au truck suit zote dark bluu
iii. T-shirt rangi ya njano.

Wasichana:

i. Raba jozi moja
ii. Bukta yenye mpira kwa chini au truck suit zote dark bluu

Vitu vingine vya kuja navyo:

2.2 Daftari kubwa kumi na moja (11), kalamu na mkebe wa hesabu
2.3 Chakula cha wanafunzi (mahindi gunia 2 na maharage debe 4 kwa muhula mmoja)
2.4 Mahitaji mengine ya kibinadamu kama nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani, pesa ya matibabu, mwamvuli, nk.
2.5 Wanafunzi wote wanaotoka nje ya kijiji cha Ntendo wanapaswa kupangishiwa nyumba katika kijiji cha Ntendo (mahali ilipo shule)
2.6 Vifaa vya usafi kama ndoo ndogo, fagio na fyekeo.

3.0 Sheria na kanuni muhimu za shule hii:-

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana na Elimu nchini chini ya **Ofisi ya Rais (TAMISEMI).** Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

(a) Heshima kwa viongozi, walimu, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kushiriki kwa makini katika kufanya maandalio ya jioni (preparations)
(d) Kuwahi katika kila shughuli na nyinginezo utakazopewa
(e) Kuwepo ndani ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
(i) Kutunza mali za umma.

3.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule:

(a) Wizi
(b) Uasherati na ushoga

(c) Ubakaji
(d) Ulevi na Matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
(e) Kupigana au kupiga
(f) Kudharau bendera ya Taifa
(g) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
(h) Kuwa mjamzito / kupata mimba
(i) kuoa au kuolewa
(j) Kutoa mimba
(k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
(l) Kukataa adhabu kwa makusudi
(m) Kuwa na simu ya mkononi

4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi ni:-
(a) **Medical Examination Form** (Fomu ya uchunguzi wa Afya ya Mwanafunzi) ambayo itatajazwa na Mganga Mkuu wa Manispaa ya Sumbawanga. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

(b) **Fomu ya Maelezo binafsi** kuhusu historia ya mwanafunzi na mktaba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(c) **Fomu ya mzazi kukiri** kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

(d) Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA LUKANGAO SEKONDARI

……..
ROBERT S. KASITU
MKUU WA SHULE

HISTORIA YA MWANAFUNZI

Jina la mwanafunzi……
Jina la baba ……..
Jina la mama ……
Shule ya msingi aliyosoma ……
Kijiji atokacho …… kitongoji cha ……
Tarehe ya kuzaliwa ……..... Dini ……Dhehebu ……..
Kabila …….

UTHIBITISHO:

5.1 Ahadi ya Mwanafunzi

Mimi …… nakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na kidato cha …… mwaka ……. Katika shule ya Sekondari Lukangao, na ninaahidi:-

i. Kuzingatia taratibu na kanuni zote za shule
ii. Kuweka bidii katika masomo yote
iii. Kushiriki katika shughuli za elimu ya kujitegemea
iv. Kuwa na nidhamu ya juu ndani na nje ya shule

Jina …….
Sahihi ……
Tarehe ……...

5.2 Ahadi ya Mzazi / Mlezi

Mimi …… mzazi / mlezi wa ……..
Naahidi kwamba:

i. Nitatimiza gharama za mwanangu kama nilivyoelekezwa
ii. Nitamhimiza mwanangu kuzingatia taratibu za shule pamoja na masomo
iii. Nakubaliana na kanuni na sheria zilizotolewa na serikali juu ya mwanafunzi (mwanangu)

Jina ……
Sahihi ……
Tarehe ……...